# RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI- KWA MWAKA 2016/2017

## SEHEMU YA KWANZA

### UTANGULIZI

Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha Kanuni cha 106 cha Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2016 na majukumu yake yametajwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni hizo kama ifuatavyo:-

(i) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliyotangulia.

(ii) Kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza.

(iii) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na miradi ya wananchi ya Wizara husika.

(iv) Kuchunguza na kufatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanya yalizingatia thamani halisi ya fedha.

(v) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.

(vi) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika

(vii) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia katika utekelezaji wa ahadi hizo.

(viii) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika

Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilianza shughuli zake za kufuatilia utekelezaji wa kazi za maendeleo ya Wizara zifuatazo:-

- Wizara ya Afya
- Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita

i) Kwa upande wa Unguja Kamati ilifanyakazi kwa muda wa wiki mbili, kuanzia tarehe 29 Agosti hadi tarehe 09 Septemba, 2016.

ii) Kwa upande wa Pemba Kamati ilifanyakazi kwa muda wa wiki mbili, kuanzia tarehe 31 Oktoba hadi tarehe 11 Novemba, 2016.

iii) Kamati iliendelea na mzunguko wa tatu wa kazi zake kwa upande wa Unguja kwa muda wa wiki mbili, kuanzia tarehe 16 hadi tarehe 27 Januari, 2017.

Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii wameshiriki kikamilifu katika kazi za kamati kwa vipindi vyote hivyo, wajumbe hao ni hawa wafuatao:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Tatu Mohammed Ussi | Makamo M/ kiti |
| 3. | Mhe. Ame Haji Ali | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Hidaya Ali Makame | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Makame Said Juma | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Masoud Abrahman Masoud | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Mjumbe |
| 9. | Ndg. Aziza Waziri Kheir | Katibu |
| 10. | Ndg. Khamis Hamadi Haji | Katibu |

**SEHEMU YA PILI**

**WIZARA YA AFYA**

Katika kipindi cha wiki tatu kati ya sita Kamati imefanyakazi ya kusimamia utekelezaji wa bajeti na shughuli za nyengine za utekelezaji katika Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2016/17 kupitia Taasisi mbali mbali za Wizara hiyo.

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ni kiungo katika Wizara hii na taasisi nyengine za Serikali ambapo Kamati ilipatiwa maelezo ya jumla kuwa Idara ina majukumu mengi yakiwemo ya kuratibu shughuli zote za Wizara pamoja na kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera ya afya, Mpango Mkakati wa Wizara, Mpango kazi na utekelezaji wa bajeti inayozingatia programu (PBB) pamoja na miongozo mengine ya afya. Miongoni mwa mafanikio yaliyofikiwa na Idara hii katika mwaka wa fedha 2016/17 ni:-

- kufanikisha kutungwa kwa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Taasisi ya Hospitali ya Mnazi mmoja ambayo inaelekea kuwa Hospitali ya Rufaa.
- kuletwa Baraza la Wawakilishi kwa Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi ambao unakusudia kuimarisha Taasisi hiyo kuwa Wakala wa Serikali unaojitegemea kwa baadhi ya mambo.

- Kukamilika Ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee ya Mkoani Pemba ambayo imeshafunguliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohammed Shein.
- Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la wodi mpya ya mama na watoto katika Hospitali ya Mnazi mmoja.

**CHANGAMOTO ZA IDARA YA SERA, MIPANGO NA UTAFITI**

Pamoja na mafanikio hayo Idara inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

1. Uhaba wa bajeti unaokwamisha utekelezaji wa baadhi ya mipango na sera kwa Wizara.
2. Upungufu wa baadhi ya wataalamu katika Sekta ya Afya hasa madaktari, Manesi na Wakunga kwa baadhi ya Hospitali na vituo vya Afya.
3. Kupungua kwa Maadili ya kazi kwa baadhi wafanyakazi wa Taasisi za Afya hasa Hospitali na vituo vya Afya.
4. Changamoto ya usafiri kwa wafanyakazi wa Hospitali ya Abdalla Mzee ambao wamehamishwa kutoka Unguja kwenda Pemba na wengine wanaishi mbali na Mkoani, hivyo kulazimika kusafiri kutoka Chake hadi Mkoani.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha bajeti ya Wizara ya Afya inaongezwa ili mipango na utekelezaji wa kazi za Wizara itekelezwe kwa ufanisi.
2. Serikali itowe kipaumbele cha ajira kwa Wataalamu Afya hasa madaktari kwa kuwawekea maslahi mazuri na vivutio vya kazi kwa waliopo.
3. Wizara iweke kanuni za maadili ya wafanyakazi kwa Hospitali na Vituo vya Afya, pamoja na kuweka mfumo rahisi wa kutoa tarifa na malalamiko kwa wananchi ambao wataona maadili ya kazi yakivunjwa na baadhi ya wafanyakazi.
4. Serikali ifanye mpango wa kuwajengea nyumba wafanyakazi wa Hospitali ya Abdalla Mzee ili kuondoa changamoto ya usafiri.

**IDARA YA HUDUMA ZA HOSPITALI**

Idara hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa upatikanaji wa huduma bora katika hospitali za Wilaya na vijiji unakua ni wa uhakika. Aidha Idara ina jukumu la kusimamia miongozo ya utoaji wa huduma za matibabu katika hospitali zote za Wilaya na vijiji kwa Unguja na Pemba, usafirishaji wa wagonjwa ndani na nje ya nchi.

Kamati ilifanya ziara katika Hospitali na vituo vya afya mbali mbali vilivyopo katika Wilaya na vijijini Unguja na Pemba ambapo changamoto na miongozo mbali mbali ilotolewa na Kamati kwa Wizara ili kuimarisha huduma za afya katika vituo na hospitali hizo. Hospitali na vituo hivyo ni kama ifuatavyo:-

**HOSPITALI YA KIVUNGE, MAKUNDUCHI, WETE VITONGOJI, KITUO CHA AFYA CHA MATEMWE, PWANI MCHANGANI, KIZIMKAZI DIMBANI, KIZIMKAZI MKUNGUNI NA MAKANGALE**

Kamati ya Ustawi wa Jamii ilifanya ziara katika Hospitali zilizotajwa hapo juu kuanzia tarehe 5/9/2016 hadi tarehe 8/9/2016 kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba kuanzia tarehe 31/10/2016 hadi tarehe 2/11/2016.

Kamati imekuta mafanikio kadhaa yamepatikana katika utoaji wa huduma za afya kwa wananchi ikiwemo ukarabati wa baadhi ya vituo mbali mbali vya afya. Hata hivyo bado zipo changamoto zinazokwamisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi. Naomba nitanabahishe kuwa katika changamoto zitakazowasilishwa katika sehemu hii, changamoto za hospitali ya Wete zinafanana na changamoto zilizopo katika kituo cha Afya Makangale, hivyo inawezekana neno kituo cha afya Makangale lisitajwe ikatajwa hospital ya Wete naomba ifahamike kuwa changamoto za hospitali hizo zinafanana ingawa hospitali ya Wete ina changamoto nyingi kubwa ukilinganisha na hospitali ya Makangale. Miongoni mwa changamoto zilizopo katika hospital hizo ni kama zifuatazo:-

1. Katika Hospitali ya Kivunge Kamati ilibaini kuwa daktari wa ganzi katika hospitali hiyo ni mmoja tu ambaye anaishi mjini na hulazimika kwenda hospitalini hapo kila siku jambo ambalo ni tatizo kwa daktari huyo na inakwamisha ufanisi katika kutoa huduma.

   Pamoja na kuwepo kwa changamoto hiyo Kamati imetambuwa kuwa tatizo hilo limewasilishwa Wizarani lakini bado mpaka siku Kamati inatembelea hospitalini ufumbuzi ulikuwa haujapatikana.

1. Hospitali na vituo vya afya vyote vilivyotembelewa na Kamati vinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa vitendea kazi kama vile majiko ya kuchemshia na vifaa vya maabara kama vile Kituo cha afya cha Matemwe na Kengeja majiko ya kuchemshia yameharibika. Kamati imebaini pia vituo vina upungufu wa dawa na jambo la kusikitisha zaidi kipindi ambacho Kamati inatembelea kulikuwa na upungufu wa dawa aina ya *panadol* katika vituo vingi. Kamati imesikitishwa sana na hali hiyo kutokana na umuhimu wa dawa hizo ambazo zimekuwa na mahitaji makubwa kwa wananchi.

2. Pia Kamati imebaini uhaba wa wafanyakazi katika vituo vingi vya afya ambapo wafanyakazi waliopo katika vituo hivyo hawatoshelezi hasa kwa kituo cha Pwani Mchangani ambacho wafanyakazi waliopo hawana nyumba ya kuishi, uhaba huo pia unavikabili vituo vya Matemwe na hospitali ya Wete.

   Kamati ilisikitishwa sana na hali iliyoikuta katika hospitali ya Wete ambapo kulikuwa na upungufu mkubwa wa wafanyakazi. Aidha, Kamati ilipata takwimu ya wafanyakazi 95 waliostaafu na kuelezwa kuwa hakuna wafanyakazi wengine waliojiriwa kuchukuwa nafasi hizo pamoja na kwamba Serikali ilitoa agizo kuwa wafanyakazi wakistaafu waajiriwe wengine.

   Ukosefu huo wa wafanyakazi unapelekea vifaa tiba vingi vilivyopo katika Hospitali hiyo kutotumika. Kamati imesikitishwa sana na hali iliyoikuta katika Hospitali ya Wete

ambapo vifaa tiba vipo vya kutosha na vimeshafungwa lakini majengo ya wodi na vifaa hivyo havitumiki kutokana na kukosekana wa wafanyakazi na kupelekea vifaa hivyo kuingia mavumbi.

Mfano wa vifaa visivyotumika ni pamoja na vifaa vya kuhifadhia watoto njiti, wodi ya ICU haitumiki na vifaa vimeshafungwa lakini hakuna madaktari na wauguzi, wodi ya akinamama waliokwisha kujifungua pia haitumiki na badala yake akinamama hao wanachanganywa na wodi nyengine kutokana na tatizo hilo hilo la ukosefu wa madaktari na wahudumu.

Kamati pia imebaini kuwa Wizara hufanya juhudi za kupeleka wafanyakazi katika hospitali hiyo lakini juhudi hizo hurudishwa nyuma na baadhi ya viongozi wa Wizara ambao wamekua wakitoa ruhusa za uhamisho kwa baadhi ya wafanyakazi na kuwarudisha Unguja kwa visingizo vya kuwa watarudi baada ya muda na wafanyakazi hao huwa hawarudi baada ya muda ulioombwa kumalizika. Upungufu wa Wauguzi pia umebainika katika chumba cha upasuaji na wakati Kamati inatembelea katika Hospitali ya Wete kulikuwa na muuguzi mmoja tu ambaye hatoshi.

3. Changamoto nyengine ni katika Hospitali ya Kivunge ambapo Kamati imebaini kuwa kwa mwezi hospitali hiyo inafanya rufaa 18 mpaka 20 jambo linalowapelekea kutumia takriban lita 400 za mafuta kwa ajili ya kuwapeleka wagonjwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

   Kamati ilielezwa changamoto iliyopo katika Hospitali ya Kivunge ambayo kwa sasa imezidiwa katika utoaji wa huduma kutokana na kuhudumiwa karibu Mkoa mzima wa Kaskazini wakati ilikusudiwa kuhudumia shehia 7 tu za Wilaya ya Kaskazini A.

   Katika Hospitali ya Kivunge Kamati ilielezwa kuwa kuna changamoto katika utoaji wa huduma za mashine ya Ultra Sound ambayo ni ndogo na haikidhi haja katika utoaji wa huduma na ni ya kuunga unga. Pia mashine ya *X-Ray* inayotumika kusafisha picha ni ya kizamani na ina madhara makubwa kwa wafanyakazi.

4. Kamati imegunduwa kuwa hospitali ya Kivunge kuna changamoto ya ukosefu wa nyumba za wafanyakazi ambapo kuna wafanyakazi 80 ambao wanahudumiwa kwa nyumba 12. Changamoto nyengine ambayo ni kubwa na takriban Kamati ilielezwa katika hospitali zote ilizotembelea ni kutopatikana kwa *"Rediation Allowances"* hali hiyo pia imebainika katika Hospitali ya Kivunge.

   Hospitali ya Kivunge kwa hivi sasa chumba cha watu wa Research ndicho kinachotumika kwa ajili ya shughuli za maabara. Kamati wakati wa ziara yake ilielezwa kuwa zinahitajika shilingi laki nane katika Hospitali ya Kivunge kwa wakati huo wa ziara katika sehemu ya maabara kwa ajili ya kifaaa cha *'Full Blood Picture Kit'*, ambacho wananchi wangeweza kukiendeleza upatikanaji wake kupitia michango. Kamati pia imebaini kuwa *X-Ray system* inayotumika ni ya kizamni hivyo ushauri wa Kamati ni kutafutwa kwa system ya kisasa ambayo itakidhi mahitaji na kutohatarisha afya za wafanyakazi ambapo ilishauri kuwa *Automatic Processor* / *Digital processor* ndiyo itakayofaa kwa sasa.

5. Aidha katika Hospitali ya Makunduchi Kamati ilipotembelea ilikuta ujenzi wa nyumba za madaktari unaendelea.

   Hata hivyo kuna changamoto ya ukosefu wa fedha ambapo kwa kipindi hicho mafundi wanaojenga ambao walikua wanajitolea walikua wanadai shilingi milioni tatu na laki saba 3,700,000/=

6. Hospitali ya Makunduchi inakabiliwa na changamoto ya kukosa wafanyakazi wa kutosha katika kuhudumia wagonjwa wanaohitaji kupata huduma ya *Ultra Sound* ambapo kuna mfanyakazi mmoja na anajitolea kufanya kazi hiyo. Aidha Kamati ilibaini kuwa mfanyakazi huyo anajitolea na anakwenda hospitalini hapo kwa siku ya Jumanne ambapo huduma za *Ultra sound* hospitalini hapo ni kwa Wilaya nzima.

7. Ukosefu wa vitendanishi ni changamoto kubwa inayozikabili maabara za Hospitali na vituo vingi vya afya vilivyotembelewea na Kamati ambapo katika hospitali ya Makunduchi mashine za *chemistry* na *hematology* nazo pia hazina vitendanishi.

8. Hospitali ya Makunduchi pia inakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa gari ya kubeba wagonjwa *(ambulance)* ya kusafirishia wagonjwa ambapo iliyopo ni moja na ni ya zamani imechoka. Aidha Kamati ilielezwa kuwa katika hospitali hiyo pia kuna changamoto ya kuharibika kwa mashine ya kufulia nguo na solar nayo haifanyi kazi

9. Changamoto ya ufinyu wa sehemu ya maabara pia inazibakabili hospitali na vituo kadhaa vya afya Kamati ilivyovitembelea, ambapo katika Kituo cha afya Matemwe na Hospitali ya Makunduchi sehemu ya maabara ni finyu mno.

10. Kamati imeona pia kuna kilio cha maslahi ya wafanyakazi wa vituo vyote vilivyotembelewa, kuna malalamiko ya ukosefu wa pesa za likizo ambapo baadhi ya wafanyakazi wanalalamika kuwa tokea walipoajiriwa hawajawahi kupatiwa pesa zao za likizo.

11. Hospitali ya Wete, Makunduchi, vituo vya afya vya Kizimkazi Dimbani na Mkunguni vinakabiliwa na ukosefu wa uzio ambapo baadhi ya hospitali na vituo hivyo, wanyama kama kuku, paka, mbuzi wanaingia ndani hasa katika Hospitali ya Makunduchi. Aidha Vituo vya Kizimkazi Dimbani na Mkunguni baadhi ya wananchi huyatumia maeneo ya vituo kwa ajili ya kuanika nyavu na matanga, walevi kukaa wakati wa usiku na kuweka vinyesi kwa baadhi ya siku kwa vile maeneo hayo yapo wazi.

12. Kituo cha Kizimkazi Mkunguni kinakosa fedha za kununulia nishati ya umeme kutokana na matumzi ya majokofu yaliyopo, pia kinakabiliwa na ukosefu wa wafanyakazi hasa wahudumu wa afya *(orderly*) ambapo kwa sasa yupo mmoja tu ambaye ni mgonjwa.

    Aidha kituo kinakabiliwa na ukosefu wa maji na hadi siku Kamati inatembelea ilibainika kuwa mota ya maji iliharibika kwa muda wa miezi minne. Pia majengo ya kituo ni mabovu ambapo jengo moja lilikarabatiwa kwa michango ya wananchi lakini yaliyobakia ni mabovu na kuna mashimo. Kituo hicho kina nyumba ya Daktari anayeishi karibu lakini nyumba hiyo ni mbovu, ina nyufa, inavuja na haifawi kwa matumizi ya binaadamu na daktari huyo anaendelea kuishi hapo katika hali duni kama hiyo.

13. Kituo cha Kizimkazi Dimbani nacho kina ukosefu wa maji, upungufu wa dawa, mashine ya kupimia wingi wa damu na B.P ilikuwa hamna ambapo mashine ya B.P iliyopo ni mashine binafsi ya Muuguzi na ilikua haina betri, uchakavu wa jengo na *ceiling board* ilikuwa inapenyeza taka na huenda ikaanguka endapo haitofanyiwa ukarabati.

    Aidha mchwa nao wanatambaa katika *hard board* na kusababisha usumbufu mkubwa hivyo wafanyakazi waliiomba Wizara iwapatiwe dawa ya kuondoa mchwa hao.

14. Pia katika kituo cha Kizimkazi Dimbani na Mkunguni Kamati ilibaini kuwa vituo hivyo vinakabiliwa na ukosefu wa walinzi wa kulinda majengo ya vituo hivyo.

15. Hospitali ya Wete imeona kuna upungufu na uchakavu wa baadhi ya vifaa katika chumba cha upasuaji na baadhi ya vifaa hivyo ni vya zamani mfano kitanda na taa ambayo haizunguki mpaka daktari asukume kitanda ili apate *'focus'* ya taa wakati wa operesheni. Vile vile kuna changamoto ya mashine ya ku *'burn'* mishipa ya damu.

    Pia Kamati imebaini kuwa kuna ukosefu wa baadhi ya vifaa vya akinamama wajawazito kama vile mipira na*'gloves'* ambavyo kwa mwaka mzima havijapatikana.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

Kutokana na changamoto nyingi zilizoanishwa hapo juu katika hospitali ya Kivunge, Makunduchi, Wete na Vituo vya Afya vya Matemwe, Pwani mchangani, Kizimkazi Dimbani na Kizimkazi Mkunguni Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao kwa Wizara:

1. Kamati inaishauri Wizara inapopelekewa changamoto hasa zile ambazo zina uhitaji mkubwa katika utoaji wa huduma kuzifanyia kazi kwa kutafuta ufumbuzi ili wananchi waweze kupata huduma kikamilifu. Tatizo la ukosefu wa daktari wa ganzi katika hospitali ya Kivunge ni changamoto kubwa ambapo Kamati inachukua nafasi hii kuishauri na kuiomba Wizara kuitatua kwa haraka.

2. Kamati inaishauri Wizara na Serikali kwa ujumla kuangalia uwezekano wa kutoa kipaumbele kikubwa katika sekta ya afya kwa kuipangia bajeti ya kutosha ili changamoto kubwa ya ukosefu wa vitendea kazi, madawa na ukosefu wa mafuta ya gari kwa baadhi ya taasisi za hospitali ziweze kupungua kwa kiasi kikubwa ili taasisi hizo ziweze kufanya wajibu wao kwa kuwahudumia wananchi ipasavyo.

    Upatikanaji wa bajeti ya kukidhi mahitaji utasababisha kukosekana sababu na visingizio vya baadhi ya watendaji wanaoshindwa kutimiza wajibu wao kwa kukosekana kwa vitendea kazi katika baadhi ya taasisi.

3. Kamati inaishauri Wizara kuzidisha juhudi za kuajiri wafanyakazi watakaoweza kuziba mapengo yaliyopo katika hospitali na vituo vya afya mbali mbali ili ile dhana ya upatikanaji wa huduma bora za afya iweze kutimia.

    Aidha Kamati inaiagiza Wizara kufanya uchunguzi wa kina kwa wahusika wote wanaochukua jukumu la kuwahamisha wafanyakazi wanaopelekwa Pemba pasi na sababu maalum na kupelekea ukosefu mkubwa wa wafanyakazi na kurudsisha nyuma

juhudi zinazochukuliwa na Serikali za kuimarisha sekta ya afya. Hivyo, Kamati inachukua nafasi hii kuwasilisha kilio hiki katika ripoti hii ili hatua za haraka ziweze kuchukuliwa na Serikali.

Aidha kutokana na maelezo yaliyotolewa kwa Kamati ya kukiukwa kwa agizo la Serikali la kujazwa nafasi zilizoachwa wazi na wastaafu, Kamati inaiagiza Wizara kulifanyia kazi agizo hilo mara moja kwa kuajiri wafanyakazi wengine watakaochukua nafasi za wastaafu kwa kufuata taratibu za sheria ya Utumishi wa Umma.

4. Kamati inashauri Wizara iongeze wataalamu katika hospitali ya Kivunge ili kuokoa muda na fedha ambazo zimekuwa zikitumika katika harakati za kufanya rufaa kwa wagonjwa na kuwapeleka katika hospitali kuu ya Mnazi Mmoja ili fedha zinazotumika kwa ajili ya mafuta zitumike kwa kununulia madawa na vifaa muhimu vya hospitali.

5. Kamati inaishauri Wizara kufanya juhudi za makusudi kutafuta wafadhili watakaotusaidia kujenga nyumba za madaktari katika vituo vya afya vilivyopo nchini ili kuondoa tatizo la makaazi kwa madaktari pamoja na kuwaondoshea usunmbufu wanaoupata hivi sasa ambapo baadhi yao hulazimika kusafiri masafa marefu kuvifuata vituo vyao vya kazi.

6. Hospitali ya Kivunge ambayo kwa sasa imezidiwa katika utoaji wa huduma kutokana na kuhudumia karibu Mkoa mzima wakati ilikusudiwa kuhudumia shehia saba, hivyo Kamati inaiomba Wizara kuboresha huduma za Hospitali hiyo kwa kuipatia vitendea kazi vitakavyoweza kukidhi mahitaji.

7. Kamati inaishauri Wizara kuimarisha huduma za vipimo vyote katika hospitali zake na vituo vya afya ili kuondosha usumbufu kwa wananchi na wafanyakazi wanaotoa huduma hizo.

8. Kamati inazidi kutoa wito kwa watendaji wakuu wa Wizara kutambua wajibu wao na wawe na utaratibu maalum wa angalau kila baada ya miezi mitatu kuvitembelea vituo vyao vya kazi kwa ajili ya kuchukua changamoto zilizopo na kuzifanyia kazi.

9. Kamati inaishauri Wizara ihakikishe upatikanaji wa vitendanishi kwa ajili ya shughuli za maabara kuwa za uhakika ili shughuli zote zinazopaswa kufanyika katika maabara hizo ziweze kutekelezwa kwa wakati. Aidha tatizo linalolalamikiwa na takriban wafanyakazi wengi wa Wizara ni posho mbali mbali, Kamati inaiagiza Wizara ilichukuwe na ilifanyie kazi pamoja na juhudi mbali mbali zilizokwisha chukuliwa katika kulitatua.

10. Kamati inaishauri Wizara na Serikali kwa ujumla kujitahidi kutafuta wafadhili watakaosaidia ujenzi wa maabara ikiwa ni pamoja na Wizara kuanza mchakato wa kutafuta maeneo maalum yatakayokuwa karibu na maeneo ya vituo vya afya kwa ajili ya kujenga maabara za kisasa zitakazosaidia kwa kiasi kikubwa upatikanaji mzuri wa huduma za afya kwa wananchi.

11. Kamati inazidi kusisitiza kwa kuishauri Wizara kujitahidi katika upatikanaji wa vitendeakazi hasa kwa hospitali na vituo vya afya vya vijijini ambavyo vinakabiliwa na ukosefu wa nyenzo za usafiri na gari za kubebea wagonjwa. Kamati pia inashauri utatuzi

wa haraka wa ukosefu wa huduma ya maji safi na salama na ukosefu wa walinzi na uzio kwa baadhi ya hospital na vituo vya afya kama vile hospital ya Wete, Makunduchi na vituo vya afya vya Kizimkazi Dimbani na Mkunguni ili kuepusha uharibufu wa mali za hospital na vituo vya afya.

**HOSPITALI YA MICHEWENI, CHAKE CHAKE, VITONGOJI, ABDALLA MZEE NA VITUO VYA AFYA KENGEJA, SHIDI NA BOGOA**

Kamati ya Ustawi wa Jamii ilifanya ziara katika Hospitali na vituo vya afya vilizotajwa hapo juu kuanzia tarehe 31/10/2016 hadi tarehe 3/11/2016 kwa upande wa Pemba. Katika ziara hiyo Kamati ilijifunza na kuona hatua kubwa zimefikiwa katika sekta ya afya kama vile kuimarisha majengo na vifaa kwa baadhi ya vituo vya afya.

Hata hivyo zipo na changamoto ambazo Wizara inapaswa izichukue na izifanyie kazi kwa kuzipunguza ili huduma za sekta ya afya ziweze kuimarika zaidi. Miongoni mwa changamoto hizo ni:-

1. Kamati ilipofanya ziara katika hospitali ya Micheweni iliridhishwa na hatua ya ukarabati wa majengo uliokuwa umefikiwa hata hivyo, changamoto kubwa ni ukosefu wa fedha wa kumalizia majengo hayo kutokana na viongozi walioahidi kusaidia ujenzi huo baadhi yao kustaafu katika siasa na kusababisha ukosefu huo wa fedha.

2. Katika hospitali ya Chake chake, Kamati ilibaini upungufu wa wafanyakazi katika sehemu mbali mbali kama vile mfanyakazi wa *jiko la kuchomea taka* ambae kwa kipindi cha ziara za Kamati alikuwepo mmoja tu na hatoshi, madereva idadi yao ni wanne tu, wanazidiwa na kazi na hawana posho la muda wa ziada wa kazi, walinzi nao wapo wanne tu hawatoshi kwa vile mpangilio wa zamu za kazi unawakosesha siku za mapumziko.

   Aidha katika kitengo cha Maabara ya Hospitali wafanyakazi wake ni wachache ambao ni sita tu na huduma zinatakiwa zitolewe saa ishirini na nne.

3. Hospitali ya Chake chake inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa baadhi ya vifaa tiba, mfano katika kitengo cha huduma ya tiba ya viungo *'physiotherapy'* mashine ya kuweka sawa viungo vya watoto ipo moja na kupelekea utoaji wa huduma kwa mashine hiyo usiwe wa ufanisi kwa vile wagonjwa wanapokuwa wengi muda wa tiba unakuwa mdogo.

   Kamati imebaini kuwa Hospitali inakabikiwa na ukosefu wa nyenzo za usafiri kwa wafanyakazi wanaotoa huduma za kifua kikuu na ukoma ambao wanatakiwa wawafikie wagonjwa majumbani mwao pamoja na ukosefu wa kinga kwa wafanyakazi hao.

   Kamati ilifahamishwa kuwa wapo baadhi ya wafanyakazi wapatao 10 wanaotoa huduma kwa wagonjwa wameambukizwa ugonjwa wa kifua kikuu katika hopitali ya Chake Chake. Vile vile wapo wafanyakazi watatu katika hospitali ya Konde wameambukizwa maradhi hayo na watoto wao na mfanyakazi mmoja wa maabara katika kituo cha afya cha Bogoa amepata maambukizi ya kifua kikuu.

Aidha, Kamati imearifiwa kuwa waafanyakazi hao wanatakiwa wafike maeneo ya vijijini kutoa huduma lakini tatizo kubwa ni nyezo za kusafiria kutoka eneo moja kwenda jengine ni tatizo ambapo hawana pikipiki imara za kufanyia kazi na zilizopo ni chakavu.

4. Kamati imeona katika hospitali ya Chake Chake kuna uchakavu wa paa la hospitali. Kwa ujumla paa la hospitali hiyo ni bovu sana na hali inasikitisha kutokana na kuvuja kwa paa hilo na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wagonjwa na wafanyakazi.

   Kamati ilishuhudia katika wodi ya akina mama, wodi ya wagonjwa wanaume, wodi ya watoto n.k, dari zake zikiwa na matundu ya ubovu na kuvujiwa, aidha wodi ya wagonjwa wa kifua kikuu wanawake haina choo Kamati imefahamishwa kuwa jengo hilo lilipofanyiwa ukarabati wakandarasi hawakumalizia kazi ya kujenga choo hicho.

5. Katika hospitali ya Chake chake pia Kamati imeona kuwa miundombinu ya maji katika maabara ya hospitali haijakaa sawa. Hali hii inasababisha maabara kukabiliwa na uhaba wa maji ya akiba. Na endapo maji yakikosekana au kuchelewa basi maabara haitaweza kuendelea na kazi mpaka isubiri huduma hiyo kutoka sehemu nyengine.

6. Hospitali ya Vitongoji nayo inakabiliwa na changamoto ya ucheleweshwaji na upungufu wa dawa muhimu kutokana na matatizo yaliyomo katika mfumo wa usambazaji wa dawa uliopo hivi sasa unaojulikana kama *'pull'* ambao unasaidia kupatikana dawa kwa mujibu wa mahitaji ya kituo lakini unachelewa.

   Kuna upungufu wa wafanyakazi ambapo Kamati imeelezwa kuwa *'radiographer'* katika hospitali hiyo yupo mmoja na wakati wa ziara ya Kamati hakuwepo alikuwa likizo na kupelekea huduma hiyo kutopatikana. Vile vile, kuna upungufu wa baadhi ya vifaa kama vile mashine za *'P.B'* ambayo kwa wakati huo wa ziara ya Kamati ilikuwepo moja nyengine zilikuwa zimeharibika, *'delivery set'* zilikuwepo tatu na zilihitajika kama kumi, '*sterilizer'* iliyokuwepo kwa wakati huo ilikuwa ni ndogo haikidhi haja.

   Pia mfumo wa maji safi na maji machafu wa hospitali ni wa zamani unahitaji matengenezo ili kuepusha kuenea kwa maradhi, kukosekana kwa huduma ya *'internet'* na kusababisha utumaji wa taarifa *'data'* kupitia mtandao kuwa mgumu, kukosekana kwa huduma ya umeme wa *'solar',* nyenzo za usafiri ni mbovu, gari la wagonjwa lililopo ni bovu, nyumba za wafanyakazi zimechakaa na zipo katika hali mbaya, baadhi ya nyumba hizo wafanyakazi wanaishi zikiwa zimeshapasuka vibaya kwa nyufa na kuhatarisha usalama wao.

7. Kituo cha afya Kengeja nacho kinachangamoto ya upungufu wa baadhi ya vifaa vya kujifungulia akina mama kama vile mipira ambayo kwa kipindi cha miezi mitatu ilikosekana, ukosefu wa daktari wa meno ingawa vifaa vya huduma hiyo vipo, upungufu wa wafanyakazi wa maabara.

   Vile vile, Kamati imeona kuwa kituo hakina usafiri wa uhakika kwa wagonjwa wanaopata rufaa na inabidi watumie gari ya Mkuu wa Kituo au mgonjwa ajitegemee pamoja na kukosekana kwa malipo ya fedha za likizo kwa wafanyakazi ambao kwa kipindi kirefu hayajalipwa.

8. Kituo cha afya Shidi kina changamoto ya ukosefu wa wafanyakazi kama vile maafisa wa afya ya jamii na mazingira kuhamasisha wananchi katika huduma za afya, tatizo la maji ambapo maji yanayotoka hayafiki ndani ya kituo, vitendea kazi visaidizi kama vile feni ambalo katika chumba cha dawa limeharibika na dawa zinapata hewa kwa kufunguliwa madirisha, mazingira ya maeneo ya kituo yanachafuliwa kutokana na wananchi kufunga wanyama wao katika maeneo ya kituo.

9. Kamati ilipotembelea katika kituo cha afya Bogoa ilielezwa kuwa maabara ya kituo inahitaji kuimarishwa kwa kupatiwa vifaa vyengine vinavyoendana na wakati wa sasa, baadhi ya vifaa na kemikali zimepitwa na wakati na havitumiki tena.

10. Kamati pia ilifanya ziara katika hospitali ya Abdalla Mzee ambapo pamoja na kuwepo majengo na vifaa vya kisasa katika Hospiali hiyo kamati ilitanabahishwa kuwa kunahitajika wafanyakazi wa kutosha wa kutoa huduma na kuvitumia vifaa hivyo, vile vile Hopitali hiyo inahitaji kuwa na umeme wa uhakika muda wote ili vifaa vya kisasa vilivyofungwa kama vile *C.T Scan* n.k viweze kudumu na kufanyakazi kwa uhakika. Kamati ilifahamishwa kuwa endapo Hospitaili haitakuwa na umeme wa uhakika vifaa hivyo vinaweza kuharibika muda mfupi.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati ilifurahishwa sana na hatua ya ujenzi iliyofikiwa katika hospitali ya Micheweni, hivyo inasisitiza Wizara ya Afya kwa kushirikiana na viongozi wa jimbo kupitia fedha za mfuko wa Jimbo kujitahidi kuchangia fedha zinazohitajika ili kumaliza ujenzi huo ili lile lengo lililokusudiwa kuifanya Hospitali hiyo kuwa ya Wilaya liweze kutimia na hatimaye ilani ya uchaguzi ya chama tawala nayo iweze kutimia.

2. Kamati inazidi kusisitiza ushauri wake kwa Wizara kuhakikisha kuwa inatoa ajira za kutosha ili kupunguza tatizo la upungufu wa madaktari na wauguzi na wataalamu wengine katika ngazi mbali mbali.

3. Kamati ilisikitishwa na taarifa iliyoipata katika hospitali ya Chake chake na hospitali nyengine kama zilivyotajwa katika changamoto zilizokumbwa na tatizo la uambukizaji wa maradhi ya kifua kikuu kwa wafanyakazi wakati wa utoaji huduma kwa wagonjwa wa maradhi hayo, ambapo na wao wakati wanatimiza majukumu yao waliambukizwa na kuhatarisha afya na uhai wao, aidha Kamati inaiagiza Wizara kufanya juhudi za makusudi kwa kuwatambua madaktari walioathirika na kuchukua hatua ya kuwatibu pamoja na kuwalipa stahiki zao zote ambazo wanastahili kulipwa.

   Kutokana na kadhia hiyo, Kamati inasisitiza umuhimu wa Wizara kufanya juhudi za kutanua baadhi ya majengo yake na kuyakarabati yale yote ambayo ni finyu na yameshachakaa. Pia Kamati inashauri Wizara ijitahidi kutafuta vifaa vya huduma ya tiba ya viungo *‘physiotherapy’* hasa mashine ya kuweka sawa viungo vya watoto.

4. Kamati inashauri hatua za haraka zichukuliwe kwa ajili ya kukarabati paa la Hospitali ya Chake Chake ili wagonjwa wapate unafuu wa afya zao na unafuu wa sehemu wanazokaa kwani hali hiyo inawavunja moyo kutokana na ukweli kwamba mgonjwa hutegemea

anapokwenda hospitali kupata nafuu lakini kutokana na hali iliyopo hospitalini hapo inawavunja moyo na kuwazidishia maradhi ambapo badala ya mgonjwa kufikiria afya yake wakati wa mvua inabidi afikirie na sehemu ya kukaa kutokana na kuvuja kwa majengo ya hospitali.

Aidha Kamati ilishangazwa na usimamizi mbovu uliofanyika wakati wa ukarabati wa jengo la wodi ya wagonjwa wa kifua kikuu wanawake kutokana na mkandarasia kutojenga choo wakati katika makubaliano ujenzi wa choo hicho ulikuwemo, kutokana na kadhia hiyo Kamati imeona kuwa huo ni uzembe wa hali ya juu na inaiagiza Wizara kufuatilia suala hilo na kuhakikisha kuwa choo hicho kinajengwa.

5. Kamati inaiagiza Wizara kutafuta tangi la maji *(tank)* na kulipeleka katika hospitali ya Chake chake kwa ajili ya kuweka maji ya akiba yatakayotumika katika maabara pamoja na maeneo yote yatakayohitaji huduma hiyo hospitalini hapo.

6. Kamati inaiagiza Wizara kuuangalia upya mfumo wake wa uombaji wa dawa kwa hospitali zake ili kuondoa tatizo linalojitokeza hivi sasa la kucheleweshwa kwa upatikanaji wa dawa muhimu ambapo tatizo hili limeikumba hospitali ya Vitongoji na nyenginezo hasa ikizingatiwa kuwa mfumo huo wa *'pull'* ambao unahitaji kituoa cha afya husika au hospitali, kupeleka mahitaji ya dawa bohari na kupatiwa dawa hizo kwa mujibu wa mahitaji, hata hivyo mfumo huo umekuwa na tatizo la ucheleweshaji wa kupatikana kwa dawa zinazoombwa licha ya maombi kuwa yanafanyika mapema na dawa zinapopatikana kunakuwa na upungufu wa dawa muhimu. Hivyo Kamati inaiagiza Wizara kuupitia tena mfumo huo ili kama una matatizo urekebishwe.

   Aidha Kamati imesikitishwa na taarifa kuwa hospitali ya vitongoji inakabiliwa na changamoto ya mfumo wa maji safi na maji machafu na kuelezwa kuwa mfumo uliopo ni wa zamani, Kamati imeshangazwa na taarifa hizo kutokana na kuamini kuwa watendaji wanaoteuliwa ni wasaidizi wakubwa wa Wizara ambao wana wajibu wa kurekebisha changamoto ndogo ndogo kama hizo ili kuondoa tatizo la maji katika hospitali.

   Hata hivyo kutokana na taarifa hiyo Kamati inaiagiza Wizara kuwasimamia watendaji wake ipasavyo ili uzembe kama huo usiendelee kuwepo na kusubiri mpaka Kamati ipite katika vituo ndipo hatua zichukuliwe wakati watendaji wenye majumuku yao wapo na wanalipwa kwa kazi hizo.

   Pia Kamati inasisitiza kama ilivyoeleza hapo awali juu ya umuhimu wa upatikaji wa makaazi ya kudumu ya madakatari ili kuwarahisishia kazi zao, pia inasisitiza kurekebishwa kwa huduma ya *internet* pamoja na kurudishwa kwa huduma ya umeme wa *solar* ili nishati ya umeme iwe ya uhakika.

7. Kutokana na changamoto Kamati iliyoikuta katika kituo cha Afya Bogoa, Kamati imeshauri kuwa ni vizuri katika miundo ya utawala kuwepo na mtu wa maabara ili aweze kufikisha na kushauri kitaalamu shughuli zinazohusu maabara na kutolewa maamuzi stahiki ambayo yatainufaisha maabara ya kituo hicho.

8. Kamati inapenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa busara wa kutafuta wafadhili ambao ni ndugu zetu wa Serikali ya China ambao walijitolea kwa hali na mali katika kuijenga upya hospitali ya Abdalla Mzee ambayo kwa kiasi kikubwa itasaidia kutatua changamoto nyingi zilizokuwa zinawakabili wananchi. Hata hivyo, Kamati ilielezwa changamoto ya ukosefu wa wafanyakazi wa kutosha ambao wataweza kuhudumia hospitalini hapo, hivyo inaiomba Serikali kama ilivyofanya jitihada za kutafuta wafadhili wa kuijenga hospitali ya Abdalla Mzee basi ihakikishe kuwa inajitahidi kupeleka wafanyakazi wa kutosha katika hospitali hiyo. Aidha Kamati baada ya kukagua jengo la hospitali hiyo inashauri mambo yafutayo:

   i. Nishati ya umeme katika jengo la hospitali ya Abdalla Mzee iwe ya uhakika na ya kudumu, baadhi ya vifaa kama vile *C.T Scan* vinahitaji umeme wa uhakika, usiokuwa wa kukatika kila mara.

   ii. Vifaa vinahitaji kufanyiwa ukaguzi mdogo na mkubwa ili kuvifanya viendelee kuwa imara.

   iii. Kusiwepo matumizi mabaya ya mashine hizo kama vile kuzifanyisha kazi kwa kupitiliza uwezo na kiasi kilichowekwa au kinachohitajika.

   iv. Kuwapa mafunzo wazawa ili waweze kuziendesha mashine hizo baada ya wataalamu wa kigeni kumaliza muda wao.

   v. Ushauri wa kitalaamu uzingatiwe katika kuendesha mashine hizo na kuzifanyia matengenezo kila inapohitajika.

   vi. Vifaa vya usalama viwekwe kama vile *CCTV* pamoja na kudumishwa hali ya usafi muda wote katika maeneo ya jengo la hospitali.

**CHUO CHA SAYANSI YA AFYA MBWENI**

Chuo Cha Sayansi ya Afya Mbweni ni miongoni mwa vyuo vinavyotoa mafunzo kwa wataalamu wetu wa fani ya afya katika ngazi tofauti tofauti. Kamati ilipata nafasi ya kufanya ziara katika chuo hicho na kujifunza mambo mbali mbali ya msingi ambayo yameweza kuisaidia Kamati katika kutimiza wajibu wake vizuri.

Pamoja na mengi mazuri yaliyopo chuoni hapo baadhi yao ni kama vile Chuo kusaidia nchi kupata wataalamu wetu wenyewe wa afya, kuwepo vifaa vya kutosha vya kufundishia, kudahili wanafunzi wenye sifa zinazotakiwa n.k. ambapo Kamati inapongeza mafanikio hayo. Kamati pia imeona changamoto zifuatazo:

1. Kamati imebaini kuwa kuna mgogoro wa ardhi ambao umedumu muda mrefu baina ya chuo na familia ya marehemu Mzee Wakati.

2. Kamati pia imefahmishwa kuwa wanafunzi wa Afya ya Mazingira wanakabiliwa na changamoto ya kukosa ajira wanapomaliza mafunzo yao.

3. Chuo cha Sayansi ya Afya kimekosa Hospitali ya Kufundishia kwa vitendo.

4. Changamoto nyengine iliyopo ambayo inawakabili wanafunzo wengi wanaokwenda kufanya mazoezi katika hospitali ya Mnazi Mmoja ni ukosefu wa vitendea kazi vingi ambavyo huwa wanafundishwa chuoni lakini Mnazi mmoja hawavikuti, aidha chuo kina uchache wa madarasa, vifaa kwa maabara na kuchakaa kwa baadhi ya vifaa vilivyomo ndani ya maabara.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati imesikitishwa sana na taarifa iliyopewa kuhusiana na mgogoro wa ardhi wa muda mrefu uliopo baina ya familia ya marehemu Mzee Wakati na Chuo, pamoja na kwamba viongozi mbali mbali pamoja na Serikali kwa ujumla wameingilia kati kutatua mgogoro huo lakini familia hiyo bado imekua ikikiuka taratibu pamoja na maamuzi yaliyokwisha fanywa.

   Kutokana na hali hiyo Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa Chuo kuweka askari wa kulilinda eneo lote la chuo kwa vile mgogoro huo umeshamalizika na yeyote atakayekiuka amri na maagizo ya kisheria yaliyotolewa hatua kali zichukuliwe dhidi yake. Aidha, Kamati inashauri eneo hilo lijengwe ukuta ili kudhibiti uvamizi.

2. Suala la ukosefu wa ajira kwa wataalamu wa masomo ya Afya ya Mazingira, Kamati inatoa ushauri kwa Wizara ishirikiane na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalumu za SMZ kwa kuzishauri Halmashauri ziwaajiri wataalamu hao na pia Wizara ijitahidi kuwaajiri katika kila kituo cha Afya.

3. Kamati inaiomba Wizara izidishe juhudi ya kuweka vifaa vingi vinavyokosekana katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ili wanafunzi wanapofanya mafunzo kwa vitendo waweze kujifunza kwa uhakika ikiwemo kuviona na kuvifanyia kazi vifaa vyote walivyojifunza wakiwa chuoni.

**HOSPITALI YA MWEMBELADU, KITUO VYA AFYA SHAKANI NA BWEFUM NA KITUO CHA DAMU SALAMA**

Kamati ilifanya ziara katika vituo na hospitali zilizotajwa hapo juu kuanzia tarehe 17/01/2017 hadi tarehe 18/01/2017 kwa lengo la kuona utekelezaji wa kazi kwa mujibu wa bajeti na sera za Wizara ya Afya. Kamati imeona vituo hivyo vinafanya majukumu yake kama kawaida na wananchi wanapata huduma za afya kadiri inavyowezekana. Hata hivyo kuna changamoto mbali mbali zinazovikabili vituo hivyo kama ifuatavyo:-

1. Katika hospitali ya wazazi ya Mwembeladu Kamati imebaini uhaba wa baadhi ya vifaa vya kuzalishia na uhaba wa baadhi ya watendaji muhimu. Vifaa vya kujifungulia kama mipira, *'gloves'* na vyenginevyo vinakuwa pungufu kwa vile huduma hizo hivi sasa zinapatikana bila ya malipo, hivyo vilitarajiwa kutolewa na Serikali lakini hata hivyo huwa havipatikani na kupelekea kutokea usumbufu kwa akinamama wanaofika Hospitali kujifungua.

   Pia Kamati iliona kuwa kuna uhaba wa wafanyakazi wa usingizi (ganzi). Vile vile, Hospitali inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa jengo la hospitali ambapo katika wodi ya wazazi imeonekana akina mama waliokwishajifungua na wanaosubiri kujifungua

wanawekwa sehemu moja wakati inatakiwa wawepo sehemu mbali mbali. Aidha chumba cha kuhifadhia mashine ya CD4 ambayo inahitaji ubaridi hakina kipoza hewa (A/C) ambapo iliyopo imeharibika, hali hii inapelekea mashine hiyo kuwa katika hali hatarishi ya kuharibika na gharama ya mashine hiyo ni kubwa.

Pia jiko la kupikia chakula ni la kizamani ambalo bado linatumia nishati ya mkaa, sambamba na hilo baadhi ya vifaa vya kufulia vimeharibika na inachukuwa muda kuvifanyia matengenezo.

2. Changamoto nyengine iliyopo katika hospitali ya Mwembeladu ni kero ya kituo cha daladala ambacho kipo mbele ya mlango wa kuingilia gari za wagonjwa, changamoto kubwa inatokea anapotokea mgonjwa wa dharura kuingia au kutoka wakati huo huo kukiwa na msongamano wa dala dala na gari nyengine mbeli ya mlango.

   Vile vile, Kamati ilipokea kilio cha takriban wafanyakazi wote cha maslahi ya wafanyakazi kuwa ni madogo na baadhi yao wakiwemo wa hospitali ya Mwembeladu kuomba kupatiwa *'night allowance'*, na fedha za sare ambazo ilielezwa kuwa wafanyakazi wananunuwa wenyewe.

   Aidha kuna changamoto ya upatikanaji wa dawa muhimu kwa watoto waliozaliwa nje ya muda (kangaroo), wazazi wanalazimika kununuwa dawa hizo na wengine hasa wanaotoka vijijini uwezo wao wa kununuwa dawa hizo ni mdogo na dawa hizo ni muhimu kwa maendeleo ya watoto hao.

3. Katika kituo cha afya Shakani Kamati imeona jengo la kituo hicho ni bovu, jengo limechimbika, linavuja na kufanya nyufa. Pia kuna tatizo la umeme kituoni hapo ambao unakatika mara kwa mara, chumba cha kuhifadhia dawa hakipo katika kiwango kinachotakiwa cha uhifadhi pamoja na maabara nayo ina changamoto hiyo hiyo.

   Kamati imefahamishwa kuwa tokea mwaka 2005 jengo hilo halijafanyiwa ukarabati, pia kituo hakina mfamasia pamoja na bwana/ bibi afya, wafanyakazi wa kituo wanaishi maeno ya mbali na hakuna usafiri wa kufika ndani kilipo kituo.

4. Kituo cha afya Bwefum nacho kina changamoto ya kukosa maji ambapo kituo kinalazimika kununua maji kwa ajili ya matumizi ya kituoni hapo, jengo la kituo linavuja na limekua finyu, ukosefu wa uzio katika maeneo ya kituo ambapo jambo hilo limepelekea kutokea kwa matukio ya wizi ambapo mara mbili yamesharipotiwa.

   Kutokana na ukosefu wa uzio, kumekuwa na maegesho ya gari za watalii kwenye eneo wazi la kituo. Kamati imebaini kuwa kituo hakina hatimiliki na kushuhudia ujenzi wa nyumba za kudumu za makaazi ya watu ndani ya eneo la kituo.

5. Kamati pia ilifanya ziara katika kituo cha damu salama na kukutana na changamoto ya upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini kuwa ni mdogo, kituo kinategemea miradi ya wafadhili ambao baadhi yao kama Marekani wameshaondoka.

   Aidha changamoto nyengine ni mwamko mdogo wa jamii katika uchangiaji damu, hapo mwanzo mwamko ulikuwa mkubwa kwa vile kituo kilikuwa kikipata msukumo wa

wafadhili lakini hivi sasa mwamko umepungua na hali hiyo inahitaji nguvu kubwa zaidi ya uhamasishaji katika uchangiaji wa damu. Kubwa zaidi Kamati imeliona ni kuharibika kwa Basi la kufatilia ukusanyaji wa damu ambapo basi hilo limepata ajali na kuharibika na linahitaji matengenezo kwa kiasi kikubwa, basi hilo ni miongoni mwa nyenzo muhimu za kufanikisha makusanyo ya damu kwa vile linaweza kufanya safari maeneo mbali mbali kwa ajili ya kukusanya damu.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inazidi kusisitiza ushauri wake kwa Wizara na Serikali kwa ujumla kuhakikisha kuwa inaajiri wafanyakazi wa kutosha katika sekta ya afya ili kukidhi mahitaji na kupunguza tatizo la ukosefu wa madaktari jambo ambalo limekuwa ni changamoto kubwa na kila hospitali na kituo cha afya kilichotembelewa na Kamati jambo hilo limekua likilalamikiwa kwa kiasi kikubwa.

   Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa upatikanaji wa vifaa vya afya muhimu pamoja na chanjo kwa watoto ili kuepusha maradhi ambayo yanaweza kuwaathiri watoto wachanga.

   Hospitali ya Mwembeladu inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa AC katika chumba cha kuhifadhia mashine ya CD4 mashine ambayo ni ya gharama kubwa, Kamati inaishauri Serikali kufanya jitihada za kunua AC kwa ajili ya chumba hicho ili kupunguza gharama ambazo zinaweza kuja kutokea endapo mashine hiyo itaharibika kutokana na ukosefu wa AC.

   Pia Kamati inaishauri Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalumu za SMZ kufanya mpango wa haraka wa kukihamisha kituo cha dala dala kilichopo mbele ya mlango wa Hospitali ya Mwembeladu ili kuondosha kero ya msongamano na usumbufu mkubwa kwa mama wajawazito wanaowahishwa kujifungua na wale wa rufaa.

   Suala la sare za wafanyakazi kujikatia wenyewe Kamati inaiagiza Wizara ilifuatilie suala hili kutokana na ukweli kuwa suala hilo ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa wafanyakazi wake wanapata sare za ofisini na kama kada nyengine wanavyofanyiwa na ofisi zao wakiwemo askari ambao wamekuwa wakipatiwa sare hizo na taasisi na sio kujinunulia wenyewe kwa pesa.

2. Kamati inaishauri Wizara ilichukue tatizo lililopo hivi sasa katika kituo cha Afya cha Shakani na katika ripoti ya mwakani Kamati itahitaji maelezo ya maendeleo ya kituo hicho ya ukarabati wake ulipofikia.

3. Kamati imefurahishwa na taarifa kuwa kituo cha Afya Bwefum kimo katika mpango wa kujengwa upya kupitia ufadhili wa washirika wa Maendeleo katika Sekta ya afya, Kamati inashauri ujenzi huo uende sammbamba na kuzuia uvamizi wa maeneo ya kituo pamoja na kukipatia kituo hicho hatimiliki ya eneo lake.

4. Kamati inaishauri Serikali kukipa kipaumbele Kituo cha damu salama kwa kukiongezea bajeti ili kiweze kujiendesha na kuondoa changamoto zilizoelezwa hasa ikizingatiwa umuhimu wa shughuli zinazofanywa kituoni hapo pamoja na umuhimu wa damu katika

Hospitali zetu. Pia Kamati inashauri basi lililopata ajali la kituo litengenezwe haraka ili liweze kufanya kazi kama ilivyokuwa mwanzo na kuepusha kuchakaa zaidi endapo litakaa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo na kuongeza gharama zisizo za lazima.

Kamati inaishauri Wizara ya Fedha kutoa umuhimu wa haraka wa kupatikana fedha za ukarabati wa basi hilo ambalo linasaidia sana kuzunguka maeneo mbali mbali kukusanya damu. Kuharibika kwa basi hilo kunapelekea zoezi la ukusanyaji wa damu kuwa na changamoto na kama tunavyojuwa kuwa akiba ya damu ni muhimu katika Hospitali zetu.

**BODI YA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI (ZFDB) NA BODI YA USHAURI HOSPITALI BINAFSI**

Mnamo tarehe 17/01/2017 Kamati ilitembelea Bodi ya Hospitali Binafsi, Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi ambapo ilipata maelezo ya kina kuhusu kazi na shughuli za Bodi hizo pamoja na mafaniko mbali mbali yaliyopatikana tokea kuanzishwa kwake. Pamoja na mambo mbali mbali ya mafanikio yaliyoelezwa kwa Kamati lakini pia kuna changamoto katika utendaji kazi wa bodi hizi, changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

1. Katika Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi ilielezwa kuwa kumekuwa na matukio ya kughushiwa kwa bidhaa na nyaraka kunakofanywa na wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu jambo ambalo limekua ni changamoto kubwa kwa bodi.

2. Uwepo wa sehemu nyingi za kificho za kuhifadhia chakula (maghala) ambayo hayatambuliki na Bodi, Pia uwepo wa bandari na njia zisizo rasmi ambazo hupitishwa chakula, dawa na vipodozi ambavyo havijakaguliwa na kuingizwa sokoni ni changamoto nyengine kubwa ambayo bodi inakabiliana nayo.

3. Kamati imefahamishwa kuwa baadhi ya wafanyabishara wanakwepa kulipa ushuru wanapoingiza bidhaa nchini pamoja na ushirikiano finyu kutoka kwa wahusika wengine. Aidha, uhaba na uchakavu wa nyenzo za usafiri unazorotesha zoezi la ufuatiliaji na ukaguzi.

4. Maslahi madogo kwa wafanyakazi wa Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi kutokana na kazi zinazofanywa na wafanyakazi hao kuwa na vishawishi vya kurubuniwa na wafanyabishara wasiokuwa waaminifu.

5. Changamoto nyengine iliyopo katika Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi ni tatizo la baadhi ya wawekezaji hasa wa mahoteli ambao wanakuja na dawa zao kutoka katika nchi zao na wakiondoka wanaziacha dawa hizo na kuanza kuuzwa katika vituo vya dawa vijijini.

6. Kwa upande wa Bodi ya Ushauri Hospitali Binafsi imeeleza changamoto zake kwa Kamati kwa kusema kuwa baadhi ya wamiliki wa Hospitali Binafsi wanakiuka miongozo na sheria za kuendesha Hopitali Binafsi. Aidha kumekua na changamoto ya kupata mashirikiano mdogo kati ya Bodi na Jeshi la Polisi wakati wa ukaguzi wa Hospitali binafsi jambo ambalo limekuwa ni usumbufu mkubwa kwa watendaji wa bodi pale wanapofungia Hospitali na vituo vya Afya visivyokidhi viwango.

7. Changamoto ya baadhi ya wamiliki kushindwa kujenga Hospitali za kisasa kutokana na kutokuwa na fedha za kufanya hivyo. Pia Bodi haina nyenzo za usafiri za kufanya ukaguzi na kufuatilia kazi zake.

8. Changamoto nyengine inayoikabili Bodi ya Ushauri Hospitali Binafsi ni udhaifu wa Sheria ya Hospitali Binafsi (Act No.4/1994) ambayo imeweka masharti yaliyopitwa na wakati ya adhabu kwa wanaovunja masharti ya sheria, kwa mfano makosa ya kutosajili daktari yamewekewa adhabu ya faini ya shilingi 7000/= ambayo imepitwa na wakati.

   Pia kutokuwepo uwiano mzuri wa malipo ya leseni kwa hospitali binafsi, kwa mfano zipo Hospitali zenye kutoa huduma kwa kiwango cha juu cha malipo kwa wagonjwa ambazo leseni yake kwa mwaka zinatozwa Tsh.200,000/= sawa na hospitali nyengine ambazo huduma zake ni za kati na kati na malipo ya huduma kwa wagonjwa ni wastani. Kamati inaona kuwa viwango hivyo vya malipo ya leseni za uendeshaji Hospitali binafsi kwa mwaka bado vidogo.

9. Wamiliki wa Hospitali binafsi wamelalamikia hatua ya taasisi za kodi kuwatoza kodi kama wafanyabiashara wakati Hospitali hizo zinasaidia kutoa huduma, wameomba Mamlaka zisaidie kuwawezesha wamudu kutoa huduma kwa kutokatwa kodi kama wafanyabishara.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inapenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi kwa mafanikio mengi iliyofikia katika utendaji wake wa kazi, hata hivyo Kamati inaiagiza Bodi kuwachukulia hatua kali wafanyabiashara wote wanaojihusisha na kughushi bidhaa na nyaraka mbali mbali kutokana na kukosa uaminifu kwa wafanyabiashara hao.

   Vile vile, Kamati pia inaiagiza Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi kwa kushirikiana na taasisi zote husika kuzidisha juhudi za ukaguzi ili iweze kuzibaini sehemu zinazotumika kuficha vyakula ambavyo havijakaguliwa na kuingizwa sokoni bila kukaguliwa.

   Kamati inachukua nafasi hii kuishauri Wizara kushirikiana na taasisi za ulinzi Serikalini na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika bandari na njia zote zisizo rasmi ambazo hutumika kupitisha vyakula, dawa na vipodozi, hivyo Kamati inaagiza wahusika wote wanaoshiriki katika kufanya vitendo hivyo wachukuliwe hatua kali kama sheria inavyoelekeza.

2. Kamati inaishauri Wizara kuipatia vifaa Bodi ya Dawa, Chakula na Vipodozi ili iweze kufanya kazi zake vizuri na kuondokana na tatizo liliopo hivi sasa la uchakavu wa vifaa, vile vile Kamati inaagiza kuchukuliwa hatua kali pamoja na kupewa adhabu kali kama sheria inavyoelekeza kwa wafanyabishara wanaokwepa kulipa ushuru wanapoingiza bidhaa nchini na wale wote wanaotoa ushirikiano finyu ili iwe fundisho kwa wengine.

3. Kamati inaagiza kuchukuliwa hatua kwa wawekezaji wote wasiofuata utaratibu uliowekwa hapa nchini hasa wawekezaji wa mahoteli wenye tabia ya kuja na dawa

kutoka katika nchi wanazotoka na wakiondoka kuziacha dawa hizo na kuanza kuuzwa katika vituo vya dawa vijijini.

4. Kamati inaiagiza Bodi ya Ushauri katika Hospitali za Binafsi kuwachukulia hatua wamiliki wote wa hospitali za binafsi wanaokiuka taratibu zilizowekwa na kuwapa adhabu kali kwa mujibu wa Sheria ili wasirudie tena tabia hiyo.

   Aidha Kamati inaishauri Wizara kuifanyia marekebisho sheria ya hospitali binafsi ambayo ni Sheria Namba 4 ya 1994 ambayo imeweka masharti yaliyopitwa na kusababisha baadhi ya wamiliki kutokua na woga wa kuvunja masharti kutokana na adhabu iliyopo kutoendana na wakati wa sasa. Kamati inasisitiza kuwa suala la uwiano wa malipo ya leseni kwa hospitali binafsi liangaliwe upya na Bodi pamoja na Wizara.

5. Kamati inashauri Wizara ya Afya kuwasiliana na kukaa na Wizara ya Fedha kutatuwa changamoto ya Wamiliki wa Hospitali binafsi ya kukatwa kodi kama ya wafanyabiashara ili kutoivunja moyo sekta binafsi ambayo inaisaidia sana Serikali kufikia lengo la kutoa huduma kwa wananchi.

**BARAZA LA WAUGUZI NA WAKUNGA ZANZIBAR NA BARAZA LA TIBA ASILI NA TIBA MBADALA**

Kamati ilikutana Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala mnamo tarehe 17/01/2017 na siku ya tarehe 18/01/2017 Kamati ilikutana na Baraza la Wauguzi na Wakunga na kupata maelezo ya kina kuhusu kazi na shughuli mbali mbali zinazofanywa na mabaraza hayo. Kwa upande wa Baraza la Wauguzi na Wakunga Kamati ilifahamu kazi zinazofanywa na Baraza hilo na kujiridhisha kuwa linafanyakazi zake kwa ufanisi na Kamati inalipongeza Baraza kwa kazi kubwa inazofanya licha ya mazingira magumu yanayowakabili.

Kwa upande wa Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala Kamati pia imefahamu kazi zinazofanywa na Baraza pamoja na jitihada mbali mbali zinazochukuliwa za kuhakikisha kuwa Baraza linaendelea kupata mafanikio katika kazi zake. Hata hivyo, katika kikao na Kamati kuna changamoto mbali mbali ambazo kamati imebaini zinakwaza utekelezaji wa kazi kwa mabaraza hayo kama ifuatavyo:-

1. Katika Baraza la Wauguzi na Wakunga Kamati imebaini kuwa kumekuwa na uchache wa walimu wenye sifa pamoja na uwepo wa vyuo ambavyo havina sifa za kutosha za kufundisha Wauguzi na Wakunga.

   Pia kuna changamoto kubwa katika maadili ya kazi kwa Wauguzi na Wakunga inayosababishwa na viwango wanavyosomeshwa wanafunzi kuwa vidogo, ukosefu wa walimu wenye sifa za kutosha, taswira hasi ya fani ya Uunguzi na Ukunga, maandalizi hafifu ya elimu ambapo wanafunzi wanakariri badala ya kuwezeshwa kufikiri wenyewe na asili ya malezi ya mwanafunzi pamoja na ukosefu wa nyenzo za kufanyia kazi ikiwemo ya usafiri.

2. Katika Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala Kamati ilielezwa kuwa kuna changamoto ya stahiki za Mrajis wa Baraza kutowekwa kwa mujibu wa nafasi yake ambayo ipo kwa mujibu wa Sheria Nam.8/2008, ingawa hatua mbali mbali zimechukuliwa na Wizara ya

Afya kusawazisha stahiki za Mrajis lakini bado suala hili halijatatuka na linaonekana kuchukuwa muda mrefu.

Pia kuna changamoto ya ufinyu wa ofisi za Baraza kwa Unguja na kutokuwepo ofisi ya Baraza kwa upande wa Pemba, sambamba na uchache wa wafanyakazi wa Baraza kwa Unguja na Pemba ambapo wafanyakazi waliokuwapo ni saba na wanaofanya kazi za Baraza ni wanne tu.

3. Kamati imefahamishwa kuwa Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala linakabiliwa na changamoto wakati wa ukaguzi hususani suala zima la usalama wa wafanyakazi katika zoezi la ukaguzi vituo na dawa asili kwa baadhi ya wahusika wanakuwa na silaha za jadi, wengine wanakuwa katika mazingira yasiyo ya kawaida (wanakuwa na mapepo kichwani), ushirikiano mdogo katika baadhi ya sehemu za ibada (misikitini) ambako baadhi ya wauza dawa asili hufanya biashara zao humo, kutokuwepo na mashirikiano endelevu na vyombo vyengine kama Baraza la Manispaa ambalo hutoa risiti kwa wauzaji wa dawa asili barabarani bila kujali kama zimekaguliwa na changamoto ya hali ya kijamii na kiasiasa ambayo wakati mwengine huathiri ufuatiliaji.

4. Kamati pia imejulishwa kuwa katika Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala kuwa kuna changamoto ya usajili wa wakunga wa jadi ambao hawaruhusiwi kuzalisha majumbani, baadhi ya sehemu za vijjini hazina huduma za hospitali au vituo vya afya vya kuzalisha kwa masaa 24, hivyo huleta usumbufu kwa mama wajawazito kujifungulia njiani wakati wakiwahishwa hospitali. Kwa utaratibu huo Baraza limetaka uhakika kama liendelee kuwasajili wakunga wa jadi au liache kuwasijili kwa vile hawaruhusiwi kuzalisha.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Mabaraza yapatiwe bajeti na fedha zinazokasimiwa katika matumizi ya Ofisi zipatikane ili kusaidia ufanisi wa kazi zao ambazo ni muhimu katika maendeleo ya Sekta ya afya.

2. Kamati imesikitishwa sana na taarifa iliyopatiwa katika Baraza la Wauguzi na Wakunga kuwa taaluma hiyo hivi sasa inakosa wataalamu waliobobea watakaoweza kuwafundisha wanafunzi wa fani hiyo maadili ambayo yatasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza kesi za mara kwa mara zinazotokea katika hospitali zetu kutokana na ukosefu wa maadili ya kazi kwa wauguzi na wakunga wengi.

   Hivyo Kamati inachukua fursa hii kuishauri Wizara kufanya juhudi za makusudi kusomesha wataalamu wazalendo na kuwapangia maslahi mazuri ili watakapomaliza kusoma waje waendeleze gurudumu la fani hiyo ambayo ni muhimu katika jamii yetu. Aidha Kamati inasisitiza upatikanaji wa vitendea kazi kwa Wizara kulipatia Baraza usafiri utakaorahisisha kazi za Baraza hilo.

3. Kamati imelipokea suala la kutowekwa kwa stahiki za mrajisi wa Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala kwa masikitiko makubwa na inaiomba Wizara isichoke kulifuatilia suala hilo hadi litakapokamilika ili stahiki ziweze kupatikana kwa mujibu wa sheria.

   Pia Kamati inaisistiza Wizara kutatua changamoto ya ufinyu wa ofisi kwa upande wa Unguja na kutafuta ofisi za Baraza kisiwani Pemba ili kazi za Barza hilo zifanyike kama

zilivyopangwa, kukosekana kwa ofisi kisiwani Pemba kunamaanisha kuwa hakuna upatikanaji wa huduma za Baraza kisiwani humo na hali hiyo inasababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaohitaji huduma za Baraza hilo.

4. Kamati inaliagiza Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala wakati wa kufanya ukaguzi katika maeneo yote washirikiane na vikosi vya ulinzi na uslama vya taifa ili kujihakikishia usalama wao, kutokana na hali hiyo Kamati inaiomba Wizara kulisaidia Baraza kuliombea ulinzi huo kwa kukutana na Wizara inayohusika na vikosi ili wakubaliane katika ngazi ya Wizara kwa lengo la kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza wakati wa zoezi hilo.

   Aidha katika kikao hicho cha Wizara mbili pia suala la Baraza la Manispaa kutoa risiti kwa wauzaji wa dawa za asili barabarani bila kujali kama zimekaguliwa dawa hizo au laa pia lijadiliwe ili muafaka upatikane na kulirahisishia Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala kazi zake.

5. Kamati inaishauri Wizara kukaa na Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala na wakubaliane kuhusiana na suala la baadhi ya wakunga wa jadi kusajiliwa au kutosajiliwa kwa vile hawaruhusiwi kuzalisha hasa ikizingatiwa kuwa kuna baadhi ya vijiji baadhi ya vituo vya afya havitoi huduma kwa muda wa saa 24.

**WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI**

Mnamo tarehe 18/01/2017 Kamati ilifanya ziara katika Ofisi ya Wakala wa Maabara ya ya Mkemia Mkuu wa Serikali na kupaa taarifa ya kina kuhusu kazi za taasisi hiyo, hata hivyo changamoto zifuatazo zilielezwa:

1. Kamati ilielezwa kuwa pamoja na ujenzi wa jengo jipya, maabara inahitaji kupatiwa vifaa vya kazi na kuongezewa vitengo vyengine vya maabara ambapo vilivyopo hivi sasa ni vitatu na vinahitajika kuwa vinane na vyote ni muhimu kwa kazi za kimaabara.

2. Pia Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu inahitaji kuwa na mpango mzuri wa kubakisha nguvu kazi yake ambayo ni ya wataalamu wanaosomeshwa kwa fedha nyingi za Serikali ambao baadhi yao huondoka kutokana na maslahi madogo yaliyopo pamoja na ukosefu wa vitendea kazi vya kisasa.

3. Kamati imebaini kuwa kuna changamoto ya stahiki za Mkemia Mkuu kuonekana kuwa kinyume na hadhi yake kama ilivyokuwa hapo mwanzo kwa watangulizi wake. Bado stahiki na hadhi ya Mkemia Mkuu haijabadilika tokea alipokuwa Mhadhiri wa Chuo Kikuu.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wizara na Serikali kwa ujumla kuwa ujenzi wa jengo jipya la maabara uzingatie na upatikanaji wa vifaa vya kazi vya kisasa pamoja na kuongeza vitengo vyengine vya maabara vyote vinavyohitajika ili kuepuka kuingia hasara mara mbili.

Vile vile, Kamati inashauri kuongeza maslahi ya wafanyakazi kutokana na ukweli kuwa wataalamu wa sekta mbali mbali ikiwemo ya afya kuwasomesha kunahitaji gharama kubwa ambapo Serikali yetu huingia gharama hizo na baada ya kumaliza masomo kwa wataalamu hao hukimbia kutokana na maslahi madogo, hivyo ili kuondoa tatizo hilo ni vyema maslahi ya wataalamu hao yakazingatiwa.

2. Kamati imesikitishwa na taarifa kuwa kuna wafanyakazi wawili waliopelekwa kusomea utalaamu wa matumzi ya mashine ya DNA ambao hadi hivi sasa mmoja hajarudi na mwengine hajulikani alipo, kutokana na kadhia hiyo Kamati inashauri kuwa Wizara ifuatilie walipo wafanyakazi hao na ikilazimika basi hatua zichukuliwe kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma.

3. Kamati inaitaka Serikali kusawazisha stahiki za Mkemia Mkuu kwa kurejesha hadhi yake kama ilivyokuwa kwa watangulizi wake.

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni miongoni mwa wizara ambazo Kamati ya Ustawi wa Jamii imezifanyia kazi mnamo tarehe 30/08/201 hadi tarehe 2/09/2016 kwa awamu ya Kwanza Upande wa Unguja na tarehe 3/11/2016 hadi 9/11/2016 kwa awamu ya kwanza upande wa Pemba.

Aidha kamati ilifanyakazi tena na Wizara mnamo tarehe 23/01/2017 hadi 27/01/2016 kwa awamu ya Pili upande wa Unguja.

Katika vipindi vyote hivyo Kamati imefatilia utekelezaji wa Progamu Kuu na Programu ndogo ndogo za Wizara kwa mujibu wa mfumo wa Bajeti inayozingatia programu. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inasimamia programu zifuatazo:-

1. PROGRAMU YA MAANDALIZI NA MSINGI
2. PROGRAMU YA ELIMU YA SEKONDARI
3. PROGRAMU YA ELIMU YA JUU
4. PROGRAM YA ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI
5. PROGRAMU YA ELIMU BORA
6. PROGRAMU YA UONGOZI NA UTAWALA

Kamati ya Ustawi wa Jamii ilipata fursa ya kufualitia utekelezaji wa Programu hizo kupitia taasisi mbali mbali zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa upande wa Unguja na Pemba katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2016/2017.

Taasisi hizo zinasimamia utekelezaji wa progamu ndogo ndogo zilimo katika programu kubwa zilizotajwa hapo juu kupitia miradi ya Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi, Uimarishaji wa Elimu ya Msingi, Uimarishaji wa Elimu ya Lazima na Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali.

Baada ya utangulizi huo, ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi katika utekelezaji wa bajeti inayozingatia programu (PBB) ambapo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inasimamia utekelezaji huo kwa progrmu sita kama ifuatavyo:-

**PROGRAMU YA ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI**

Programu hii inahusu utoaji wa elimu ya maandalizi na msingi kwa wanafunzi wenye umri kati ya miaka minne hadi kumi na moja. Katika utekelezaji wa bajeti kwa robo mbili za mwaka wa fedha 2016/17 Wizara imefanya kazi kubwa ya kuimarisha nyenzo na mazingira ya kujifunza, mafunzo ya walimu na miundombinu ya kusoma na kusomeshea kwa skuli za msingi na maandalizi.

**CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU**

Katika utekelezaji wa Programu hii licha ya mafanikio kufikiwa kamati imeona changamoto mbali mbali ambazo zinatakiwa kufanyiwa kazi kuzitatua kama ifuatavyo:-

1. Ukosefu wa huduma za lazima kwenye Skuli za Maandalizi na Msingi; changamoto hii ni kubwa katika Skuli ya Maandalizi ya Madungu-Chake Chake kuna tatizo kubwa la huduma ya maji ukizingatia wapo watoto wadogo wengi wanasoma, aidha Skuli nyingi Pemba zimekuwa zinakumbwa na tatizo la uhaba au ukosefu wa huduma ya maji. Kuna matatizo ya ubovu wa vyoo katika Skuli ya Darajani Unguja na skuli mbali mbali.

2. Uchakavu wa Miundombinu na mazingira duni ya Skuli; changamoto hii inahusu uchakavu wa majengo ya baadhi ya Skuli kama vile Kiuyu Minungwini kuna majengo yamekuwa mabovu na mengine yanahitaji kujengwa upya, skuli ya Darajani majengo yake yanavuja, sakafu za madarasa zimekuwa mbovu na kuna matatizo ya vikalio kwa Skuli nyingi za msingi.

   Skuli ya Maandalizi ya Madungu eneo lake halina uzio, inatoa fursa kwa wahalifu kuweka masikani yao kufanya vitendo vya kihuni kama kuvuta bangi, uasharati na ulevi mambo ambayo ni hatari kwa mazingira yanayohusu watoto.

3. Matatizo ya utoro wa wanafunzi, wingi wa wanafunzi kwenye madarasa na uchache wa walimu wa Maandalizi na msingi. Changamto hii ni kubwa zipo skuli kamati imetembelea idadi ya wanafunzi madarasani ni wengi sana wanafika 100 kwa darasa hasa madarasa ya kwanza (STD I) huku walimu wakiwa wachache. Vile vile kuna changamoto ya utoro wa wanafunzi hasa skuli zilizopo katika ukanda wa pwani.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Huduma za lazima na Miundombinu ziimarishwe katika Skuli za Maandalizi na Msingi. Upatakinaji wa huduma za lazima kama maji, vyoo na usalama wa skuli uhakikishwe kwa kushirikiana na mamlaka zinazotoa huduma hizo pamoja na upatikanaji wa fedha za bajeti.

2. Majengo ya Skuli yafanyiwe ukarabati pamoja na kuwekwa uzio kwa maeneo yenye hali duni ya usalama mfano Skuli ya Maandalizi ya Madungu.

3. Utafiti ufanyike kujua njia za kudhibiti utoro wa wanafunzi hasa katika skuli za ukanda wa pwani zenye shughuli nyingi za uvuvi na utalii, pamoja na kudhibiti wingi wa wanafunzi madarasani kwa kujenga madarasa mapya na kuajiri walimu wa msingi wa kutosha.

## PROGRAMU YA ELIMU YA SEKONDARI

Programu hii inahusu usimamizi wa elimu ya Sekondari kwa vijana wenye umri kati ya miaka 12 hadi 17. Katika robo mbili za mwaka wa fedha 2016/17 hatua kubwa zimefikiwa katika utekelezaji wa programu kama vile kuimarisha miundombinu ya skuli kwa ujenzi kukamilisha miradi ya skuli za Sekondari za kisasa kila Mkoa, upatikanaji wa vifaa vya skuli, madawati n.k

## CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU

Pamoja na mafanikio hayo changamoto mbali mbali zimejitokeza katika utekelezaji wa programu hiyo kama ifuatavyo:-

1. Matokeo yasiyoridhisha katika mitihani ya kitaifa; licha ya juhudi kubwa za Wizara katika kuimarisha elimu ya Sekondari bado Skuli za Sekondari za Zanzibar hazipati matokeo ya kuridhisha katika mitihani ya kidato cha nne na sita kitaifa. Ingawa kunahitajika kufanywa utafiti zaidi lakini kamati imetembelea Skuli kadhaa za Sekondari Unguja na Pemba na kwa muda mfupi imeona yafuatayo kuwa yanachangia upatikanaji wa matokeo yasiyoridhisha kwa skuli za Zanzibar:-

   a. Uhaba wa walimu wa kutosha wa Sekondari wenye uweledi wa kufundisha, mbinu na maadili, sambamba na uhaba wa walimu wa masomo ya Sayansi katika Skuli nyingi za Sekondari Unguja na Pemba, mfano Skuli ya Sekondari ya Kiuyu Minungwini haikuwa na mwalimu wa somo la Baolojia wakati wanafunzi wanasubiri kulifanyia mtihani wa kidato cha nne somo hilo.

   b. Uhaba wa vitabu na vifaa vya kufundishia; kutopatikana kwa vifaa kama vile vya maabara kwa wakati kunarudisha nyuma ufaulu wa wanafunzi, baadhi ya skuli wanapata vifaa vya maabara miezi mitatu kabla ya mtihani wa kitaifa wanafunzi wanashindwa ufanisi. Baadhi ya skuli hazina vikalio kwa wanafunzi mfano skuli ya Tumekuja baadhi ya wanafunzi wa Sekondari wanakaa chini.

   c. Ukosefu wa dakhalia za kutosha unawanyima wanafunzi wa Zanzibar mazingira tulivu ya kusoma. Wanafunzi wengi wanatoka maeneo ya mbali na wanasumbuka katika usafiri wa gari za abira, wengine wanaishi kwa jamaa zao ambao hali zao kimaisha ni duni.

   d. Huduma hazitoshelezi katika Skuli za Sekondari zenye dakhalia; baadhi ya skuli zenye dakhalia kama vile Utaani na Chasasa Wete hazina usafiri kwa wanafunzi wanapopatwa matatizo na nyengine za mjini Unguja wanafunzi wanapata changamoto ya huduma za chakula.

2. Changamoto ya miundombuni ya Skuli na huduma za lazima; baadhi ya majengo ya Skuli za Sekondari yanavuja mfano Skuli ya Sekondari ya Maendeleo Ngwachani, na maabara za skuli ya Lumumba zinavujiwa.

   Kuna changamoto ya huduma ya maji baadhi ya skuli mfano skuli za Lumumba, Tumekuja, Ufundi Kengeja na Maendeleo Ngwachani. Kamati imekuta changamoto ya kufikishwa maji katika Skuli mpya ya Sekondari ya kisasa ya Mkanyageni.

   Kuna baadhi ya Skuli zanahitaji kuwekwa uzio ili kuimarisha usalama wa mali za skuli na wanafunzi mfano skuli ya Ufundi Kengeja, Utaani na Chasasa.

3. Skuli za Sekondari za Ufundi zinahitaji kuongezewa vifaa, walimu na fani mpya za kufundishwa kwa mfano Skuli ya Ufundi Kengeja inachangamoto kama hizo.

4. Baadhi ya Skuli za Sekondari zina uhaba wa madarasa na zinahitaji kuongezewa nguvu ya ujenzi wa madarasa mapya, mfano Skuli ya Uweleni ya Mkoani inahitaji kuongezwa nguvu ya kumalizia ujenzi wa madarasa na ukumbi ambao umejengwa kwa nguvu za wazee.

   Aidha, Skuli hiyo inahitaji kujengewa uzio pamoja na kuondoa vibanda vya wafanyabishara waliobakia kando ya skuli.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Katika kukuza viwango vya ufaulu kwa Skuli zetu:-

   a. Mfumo wa Elimu ya Maandalizi na Msingi upitiwe na kuimarishwa zaidi kwa kuhakikisha wanafunzi wanaotoka maandalizi kwenda msingi wana uwezo wa kusoma, kuandika na kuhesabu vizuri na wanafunzi wanaotoka msingi kwenda Sekondari wanakuwa na uwezo zaidi wa ufahamu.

      Vile vile, madarasa ya msingi na maandalizi yasiwe na idadi kubwa ya wanafunzi kupitiliza ili walimu wawe na uwezo wa kumudu kufundisha kwa ufanisi. Walimu wa maandalizi na msingi wapatiwe mafunzo na nyenzo za kufundishia kwa mujibu wa mahitaji ya maandalizi na msingi, na wanafunzi wa maandalizi na msingi wapatiwe vikalio na vifaa vya kujifunzia mapema ili waweze kutumia karama na ujuzi wakiwa bado wadogo.

   b. Mashirikiano baina ya wazee, walimu na wanafunzi yawe jambo la lazima kuanzia maandalizi, msingi na Sekondari kwa kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi akiwa nyumbani, skuli na maeneo ya kujifunza kama maktaba.

   c. Serikali kupitia Wizara ye Elimu ihakikishe walimu wa kutosha wanapatikana wakiwa na sifa na uwezo wa kufundisha, mbinu na maadili. Walimu wa masomo ya Sayansi wa kutosha waajiriwe, maslahi na mazingira mazuri ya kufanyakazi kwa walimu yaimarishwe.

   d. Vitabu na vifaa vya maabara vipatikane kwa wakati badala ya wanafunzi kupatiwa vifaa hivyo miezi michache kabla ya kufanya mtihani.

e. Serikali irejeshe dakhalia kama ilivyokuwa zamani ili kuweka mazingira tulivu ya wanafunzi kujisomea. Uwekezaji katika sekta ya elimu unahitaji gharama hivyo Serikali ifanye kila inaloweza kurudisha dakhali kwa maslahi ya elimu yetu.

f. Skuli za Msingi na Sekondari zipatiwe maktaba na vitabu ili kutanua wigo wa kujiongezea maarifa kwa walimu na wanafunzi, aidha Serikali ifanye mpango wa kuanzisha mradi wa kujenga Maktaba katika kila Mkoa na Wilaya.

2. Miundombinu na huduma za lazima katika skuli ifanyiwe ukarabati kwa upande wa majengo, kuzipatia huduma za maji, umeme na usalama katika maeneo ya Skuli. Aidha Serikali ifanye mpango wa kuhakisha usalama kwa majengo ya skuli yaliyochakaa hasa Mji Mkongwe.

3. Skuli za Sekondari za Ufundi ziimarishwe kwa kupatiwa vifaa, mazingira ya kusoma na kusomesha, fani za masomo ziongezwe kwa mujibu wa mahitaji ya hivi sasa ya soko la ajira, walimu wa Skuli za Ufundi wapatiwe motisha ili waendee kubakia kwa kuwa wengi wao wanakimbia kwa sababu mbali mbali ikiwemo maslahi duni.

**PROGRAMU YA ELIMU YA JUU**

Programu ya Elimu ya Juu kwa ujumla inahusu uratibu wa elimu ya juu na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) pamoja na utoaji wa huduma ya mikopo kwa wanafunzi wanaojiunga na elimu ya juu.

Kamati imeona kazi kubwa imefanyika ya utekelezaji wa programu hii katika robo mbili za mwaka wa fedha 2016/17 kama vile ujenzi wa jengo jipya la Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia upo katika hatua nzuri, mpango wa kununu vifaa vipya vya kufundishia katika Taasisi unaendelea.

Mpango huo wa ununuzi wa vifaa pia unafanyika SUZA na zoezi la urejeshaji mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu linaonekana kupiga hatua nzuri. Kamati imeona maendeleo yaliyopatikana katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ambacho idadi ya wanafunzi wanaoingia pamoja na vitivo inaongezeka kila mwaka.

**CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU**

Pamoja na mafanikio hayo kamati imeona changamoto kadhaa zinakabili utekelezaji wa programu hii katika taasisi mbali mbali kama ifuatavyo:-

1. Uhaba wa bajeti unaathiri mipango ya maendeleo ya elimu ya juu kwa baadhi ya vyuo vya Serikali. Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) hakipati fedha za Maendeleo katika bajeti yake na kuchelewesha utekelezaji wa mipango yake muhimu kama vile ujenzi wa mabweni na ukumbi wa mahafali.

   Taasisi ya Kurume ya Sayansi (KIST) inahitaji kuongezewa bajeti ili iweze kuendeleza fani inazotoa katika ngazi ya shahada, kuendeleza walimu wake na kufanya tafiti. Vyuo vinahitaji kuimarishwa huduma za dakhalia, majengo, mahitaji ya wanafunzi na usafiri.

2. Ukarabati wa majengo na Miundombinu; Chuo cha Kiislamu Micheweni kinakabiliwa na tatizo la kuvujiwa majengo yote. Vile vile, Chuo hiki kinahitaji kuendelezwa ujenzi wa uzio uliokwama kwasababu ya vikwazo vya baadhi ya wanajamii wa Micheweni kukataa kujengwa kwa uzio huo.

   Tawi la SUZA Mchangamdogo kunahitaji kujengwa uzio ili kulinda majengo na mali za Chuo. Sambamba na vyuo hivyo, jengo la Ofisi ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ni finyu mno halikidhi mahitaji ya Bodi kama vile uhifadhi wa kumbukumbu za wakopaji.

3. Maslahi madogo ya walimu wa vyuo na mazingira duni ya kufanyakazi; maslahi ya walimu wa vyuo ni madogo, wengi wanaondoka na kutafuta vyuo vyengine binafsi kufanyakazi, walimu wa SUZA tawi la Mchangamdogo wanahitaji kurekebishiwa mishahara yao ambayo kwa muda mrefu hawajarekebishiwa kulingana na viwango vya SUZA. Walimu wa Chuo cha Kiislamu Micheweni hawana nyumba za kuishi na wanajibanza kwenye nyumba moja walimu wanne.

4. Upatikanaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu unachangamoto wanafunzi wengi wanakosa wakati baadhi wanapata mara mbili kwa Bodi ya Mikopo ya Bara na Zanzibar.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Bajeti za Vyuo vya Elimu ya Juu iongezwe kwa kuvipatia vyuo ruzuku/fedha za maendeleo ili vikamilishe prograumu zake mbali mbali ambazo nyingi haziwezi kusubiri mpaka hali ya fedha iwe nzuri sana mfano ujenzi wa mabweni na mpango wa kuanzisha shada ya kwanza ya masomo ya ufundi kwa Taasisi ya Sayansi ya Karume (KIST).

2. Majengo na miundombinu ya Vyuo ikarabitiwe ili kuimarisha mazingira ya usomeshaji, aidha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu inahitaji kupatiwa jengo la kutosha kukidhi mahitaji ya kiofisi hasa uhifadhi wa kumbukumbu za wakopaji, jengo linalotumiwa sasa na Bodi hiyo ni finyu mno hata ukumbi wa mikutano halina.

3. Walimu wa vyuo wapatiwe maslahi yao inavyostahiki na nyumba za kuishi au nyenzo za usafiri za uhakika kuwawezesha kufanyakazi yao vizuri.

4. Dakhalia za wanafunzi ziimarishwe na huduma za dakhalia zipatikane ili wanafunzi wasome kwanye mazingira yenye utulivu.

5. Mgogoro kati ya wanajamii wa Micheweni na Chuo cha Kiislamu Micheweni upatiwe ufumbuzi wa kudumu ili Ujenzi wa uzio wa Chuo uendelee.

6. Serikali ibuni vyanzo vya kupata fedha za kuwakopesha wanafunzi wa elimu ya juu ambao wengi wao wanasifa za kuendelea lakini wanakosa mikopo kutokana na uhaba wa fedha. Utaratibu wa kurejesha mikopo uende sambasamba na kiasi cha mshahara cha mkopaji na hali ya uchumi, wapo wanafunzi waliokopa wanalalamika makato ya mkopo ni makubwa wakati mishahara ni midogo na huku hali ya maisha ikiwa ngumu.

**PROGRAMU YA ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI**

Katika utekelezaji wa Programu hii Kamati imeona mafanikio yaliyopatikana ni makubwa kwanza vituo vingi vimejengwa vizuri, walimu wanafanyakazi kwa bidii, wanafunzi wengi wanajiunga na kumaliza masomo yao wakiwa na ujuzi na wengine kujiari na baadhi yao wanamudu ushindani wa soko la ajira kwa ujizu walionao.

**CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU**

Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana zipo changamoto kama ifuatavyo:-

1. Vyuo vya Amali vinakabiliwa na uhaba wa fedha za kuendesha mipango na programu zao mbali mbali ambazo zikifanikiwa zitawezesha vijana kujiajiri na kuipunguzia Serikali mzigo wa kuajiri.

2. Vyuo vinakabiliwa na upungufu wa vifaa vya kusomeshea na nyenzo za kufanya kazi za vitendo kwa wanafunzi. Vifaa vinavyohitika kama vile mashine na mitambo, vyarahani, majiko, kompyuta, vifaa vya umeme, vifaa vya usaramala. Na nyenzo za kufanyia kazi kama vile vitambaa, mbao, vyuma, waya, gari chakavu za kufanyia mazoezi n.k

3. Maslahi ya walimu wa vyuo vya amali na mafuzo mbadala ni madogo kulingana na kazi wanazofanya za kuwapa ujuzi wa vitendo wanafunzi.

4. Uchakavu wa majengo wa baadhi ya vituo na miundombinu; majengo ya vituo vya elimu mbadala kama vile vya Forodhani yamekuwa chakavu, jengo la kituo cha elimu mbadala Rahaleo linahitaji kupatiwa kuwepo na majengo ya kutosha ya karakana. Kituo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni eneo lake linavamiwa na wakaazi hivyo kunahitaji kujengwa uzio.

5. Changamoto ya dakhalia hasa kwa wanafunzi wa vyuo vya amali; Chuo cha Amali cha Vitongoji kinajitaji kuwekwa ukuta hasa kwa dakhalia ya wanawake ambayo ipo karibu na dakhalia za Skuli ya Fidel Castro, wanapata usumbufu wa kuvamiwa na baadhi ya watu nyakati za usiku kwa vile dakhalia hizo hazina uzio.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Vyuo vya Amali na Vituo vya elimu mbadala vipatiwe fedha za kutosha za kuendesha programu zake na upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na mazowezi ya wanafunzi. Kamati inashauri sana fedha za *"Skill Development Levy" (SDL)* zilizotungiwa sheria na Baraza la Wawakilishi na ambazo zinakusanywa kwa michango ya vyuo vyenyewe hasa vyuo binafsi, zipatikane na kupatiwa vyuo vya Amali na Mbadala. Kamati imebaini kuwa fedha hizo hazijawahi kutolewa kwa vyuo hivyo hata mara moja.

2. Majengo na Miundombinu ya vyuo na vitu vya amali yafanyiwe ukarabati ili mazingira ya kusomea yawe mazuri hasa kituo cha Forodhani ambacho hali ya Majengo yake ni chakavu na Kamati inapendekeza mpango ufanyike kujengewa majengo mengine.

3. Juhudi za lazima na za makusudi zifanywe kujenga uzio wa dakhali ya wa wanafunzi wanawake katika Chuo cha Amali cha Vitongoji ili kulinda usalama wao kutokana na vitendo vya baadhi ya watu wanaowavamia nyakati za usiku.

4. Maslahi ya walimu wa Vyuo na Vituo vya Amali yaimarishwe kwa kuwa wanajitolea sana kusomesha wanafunzi kazi za vitendo ambazo ni ngumu na zina changamoto mbali mbali, aidha vyuo vipatiwe usafiri kwa kazi zake mbali mbali za ufuatiliaji.

5. Wanafunzi wa wapatiwe nyenzo za kufanyia mazowezi; Kamati inashauri Shirika la Bima la Zanzibar kusaidia kuwapatia Chuo cha Amali Mkokotoni gari zilizoharibika kwenye ajali ili wanafunzi wafanye mazowezi ya ufundi ya ukarabati wa gari hizo.

**PROGRAMU YA UBORA WA ELIMU**

Programu hii inahusu jukumu la Wizara kuhakikisha elimu inayotolewa ni yenye ubora unaokubalika katika jamii, kikanda na kimataifa ili kuwezesha wanafunzi kumudu ushindani katika soko la ajira.

Mwaka wa fedha 2016/17 hatua mbali mbali za kuridhidha zimefikiwa katika utelezaji kubwa zaidi ni hatua ya Wizara kuweza kuwalipa kwa wakati walimu waliosimamia na kusainisha mitihani, kukamilisha zoezi la kuwapima wanafunzi, kufanya mafunzo ya TEHAMA kwa walimu na ukutubi kwa wafanyakazi wa maktaba kuu, mafunzo ya watendaji wa kituo cha habari elimu Kwarara n.k

**CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU**

1. Kumekuwa na malalamiko ya uratibu wa mitihani ya ***“mock”*** ambayo inadaiwa kuwa inavuja na haitowi vimipo vizuri kwa wanafunzi.

2. Upatikanaji wa fedha kwa wakati unaleta changamoto ya kushindwa kupanga ratiba ya mtihani kwa wakati.

3. Changamoto katika kambi ya kusanisha mitihani kuhusu huduma za chakula na malazi kuwa duni. Vile vile, katika zoezi la kusimamia mitihani kunakosekana mazingatio ya uwezeshaji kwa walimu wanaosimamia mitihani katika maeneo yenye changamoto maalumu kama vile Tumbatu na Uzi, kupatiwa malipo sawa na walimu wanaosimamia mitihani katika maeneo mengine mfano Kiswandui.

4. Mashirikiano hafifu baina ya wazee na wanafunzi yanazorotesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi.

5. Wizi wa vitabu katika Shirika la Huduma za Maktaba na hatua dhaifu za jeshi la Polisi kushughulikia wahalifu wanaokamatwa kwa kuwaachia huru. Aidha baadhi ya vitabu vya Serikali vinauzwa kinyume cha Sheria katika maduka ya vitabu na wahusika wapokamatwa hatua za kisheria zinakuwa dhaifu dhidi yao. Vile vile, Shirika la Huduma za Maktaba halina gari na vifaa kama nyenzo kama kompyuta hakuna katika Maktaba ya Pemba.

6. Vituo vya Walimu (TCs) vinakabiliwa na Changamoto kubwa ya kutofikishiwa bajeti na badala yake vituo hivyo vinategemea kuendesha shughuli zake kwa fedha za michango ya miradi yake ya ndani, michango ya walimu na wanafunzi ambayo imepungua baada ya kufutwa michango katika skuli za msingi. Vituo hivi pia vinakabiliwa na matatizo ya usafiri.

7. Ukaguzi wa Walimu inaonekana kutokuwa wa ufanisi kwa vile unachukuwa muda kutokana na ukosefu wa fedha za usafiri.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Baraza la Mitihani lipewe jukumu kikamilifu kusimamia mitihani ya "Mock" ili kuwe na uratibu mmoja tu utakaodhibiti mapungufu katika mitihani hiyo. Aidha fedha za bajeti zipatikane mapema ili Baraza lipange ratiba ya mtihani kwa wakati.

2. Changamoto za kusimamia mitihani na kambi ya kusainisha mitihani zipatiwe ufumbuzi kwa kuwa hayo yanawezekana ndani ya Wizara yenyewe.

3. Serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ichukuwe hatua kwa kukaa na jeshi la Polisi kuelekezana utaratibu thabiti wa hatua za kisheria kwa wale wote wanaokamatwa wakiiba na kuuza vitabu vya Serikali ambao jeshi la Polisi halichukuwi hatua madhubuti wanapokamatwa. Kamati pia inashauri Maktaba ipatiwe usafiri na vifaa vya Kompyuta kwa upande wa Pemba.

4. Vituo vya Ualimu (TCs) vipatiwe fedha za bajeti ili shughuli zake ziweze kufanyika kwa ufanisi badala ya kutegemea michango ya walimu na wazee ambayo haipatikani kwa ukamilifu. Aidha, vituo vipatiwe usafiri wa uhakika ili viweze kufatilia walimu katika skuli zao.

5. Wizara iweke bajeti ya kutosha na kuhakikisha kuwa Ukaguzi unafanyika mara kwa mara ili kujuwa uwezo wa walimu katika kazi zao na kurekebisha makosa kwa wakati.

**PROGRAMU YA UONGOZI NA UTAWALA**

Programu hii inahusu usimamizi wa shughuli zote za Sekta ya Elimu ikijumuisha mipango, será na tafiti za kielimu, uendeshaji na utumishi na uratibu wa shughuli za elimu kwa upande wa Pemba.

Katika robo mbili za mwaka wa fedha 2016/17 programu ilitekeleza kazi mbali mbali kama vile kutayarisha mpango mkuu wa elimu wa miaka mitano (2016-2020), toleo la matokeo ya utafiti kwa walimu wa Skuli za Msingi, matayarisho ya kitabu cha takwimu, mafunzo kwa kamati za wazee kwa skuli mbali mbali za Unguja na Pemba, kuchapisha kiongozi cha majukumu ya walimu wakuu na maafisa wa elimu Wilaya.

**CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU**

1. Ufikishwaji wa fedha za bajeti katika shughuli mbali mbali za elimu kama vile mafunzo ya walimu, vitendea kazi, vifaa vya kufundishia ambavyo huwekwa katika bajeti lakini fedha hizo hazifi inavyopasa.

2. Kuchelewa kwa baadhi ya wakandarasi kukamisha kwa wakati kazi katika miradi ya ujenzi mfano ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya kisasa ya Kibuteni hauna maendeleo mazuri.

   Wakati Kamati inatayarisha ripoti hii ilifanya ziara ya kutembelea eneo la ujenzi mnamo tarehe 10/2/2017 na imeona hakuna kazi inayoendelea katika eneo hilo ambalo hivi sasa limeachwa na walinzi tu. Ujenzi huu umeanza sambamba na ule wa Skuli ya Sekondari ya Kisasa ya Mkanyageni Pemba ambao umeshakamilika na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar ameshaifungua rasmi.

   Ujenzi wa Chuo cha Amali cha Kigaeni Makunduchi umechelewa kuanza kwasababu mbali mbali ikiwemo kuchelewa kwa mshauri elekezi kuanza kazi. Hata hivyo, mnamo tarehe 10/2/2017 Kamati imetembelea tena na kukuta ujenzi huo katika hatua ya kusimamishwa nguzo na kufukiwa. Kamati imefahamishwa kuwa maendeleo ya ujenzi huo kumalizika kwa wakati yanaweza kuathiriwa na hali ya upungufu wa mchanga wa kujengea inayoendelea nchini.

3. Changamoto ya ajira kwa walimu wa masomo ya Sayansi, Ufundi na Mafunzo ya Amali. Skuli nyingi zina upungufu wa walimu wa Sayansi, aidha walimu wa masomo ya ufundi na amali wanahitaji kuendelezwa kwa kupatiwa mafunzo zaidi.

4. Ukosefu wa huduma za maktaba kwa skuli za msingi na Sekondari na katika jamii kwa ujumla, kunazorotesha mwamko wa wanafunzi na jamii kujiongezea maarifa.

5. Uhaba wa nafasi kwa madarasa ya maandalizi na msingi, na kupelekea msongamano wa idadi kubwa ya wanafunzi katika darasa moja.

6. Ukosefu wa wakutubi na wasaidizi wa maabara katika Skuli za Sekondari.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kwa kuwa elimu ndiyo mkombozi wa taifa na maendeleo, Serikali ihakikishe inaongeza bajeti yake kwa Wizara ya Elimu na kuhakikisha kuwa kasma inayopangwa (O/C) inapatikana ya kutosha ili shughuli muhimu na kazi zinazotaka kutekelezwa zisikwame.

2. Serikali kupitia Wizara ya Elimu iwe makini katika kutafuta wakandarasi na washauri elekezi katika miradi ya ujenzi, na katika miradi yenye wafadhili yawepo majadiliano ya pamoja na wafadhili wa miradi hiyo katika kuweka vigezo vya kupata wakandarasi na washauri elekezi ambao hawatachelewesha kukamilika kwa miradi ya ujenzi.

3. Mkakati maalumu wa kuhakikisha Skuli zinapata walimu bora wa Sayansi upangwe kwa kuongeza maslahi zaidi na kuwapatia mafunzo na mbinu bora za ufundishaji walimu waliopo sasa, mpango huu pia utafanikiwa kwa kupatiwa fedha, nyenzo na usafiri kwa vituo vya Ualimu (TCs).

4. Serikali itafute wafadhili kujenga Maktaba katika kila Mkoa ili kutanua wigo wa kujiongezea maarifa, Vile vile, Wizara itowe kipaumbele cha ujenzi wa madarasa ya maandalizi na msingi ili kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani.

5. Serikali itowe fursa za ajira kwa wakutubi na wasaidizi maabara katika Skuli za Sekondari badala ya kutumia walimu wa kawaida kufanya kazi hizo huku walimu hao wakiwa na vipindi vya kusomesha madarasani.

**SEHEMU YA TATU**

**HITIMISHO**

Katika kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Kanuni za Baraza la Wawakilishi na Sheria nyenginezo, Kamati imetoa maelekezo na ushauri wake ambao tunaamini kuwa utasaidia katika kuleta ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu ya Serikali kupitia ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Maelekezo na maoni hayo yalitolewa na Kamati kwa dhamira ya kuwawakilisha vyema wananchi wa Zanzibar na kuona kuwa maslahi ya wananchi hao, kwa mujibu wa sheria yanapewa kipaumbele.

Kamati yetu inatumai kuwa maelekezo na maoni yaliyotolewa na Kamati kwa Wizara hizo yatazingatiwa kwa lengo la kutoa huduma zilizotukuka kwa wananchi wa Zanzibar. Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwanza kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake vizuri, lakini zaidi kwa ushauri walioupatia Kamati yetu katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yake.

XXXXXXXXXXXXXX *MWISHO* XXXXXXXXXXXX